# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

## MUHTASARI WA MAFUNZO YA UALIMU NGAZI YA CHETI
## ELIMU KWA MICHEZO

## SOMO LA UALIMU

**2009**

©  Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, 2009

ISBN…………………………………………………..

Haki zote zimehifadhiwa.  Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kupiga chapa au kutoa kwa namna yoyote ile muhutasari huu bila idhini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Muhtasari huu  na umeandaliwa na:
Taasisi ya Elimu Tanzania
P. O. Box 35094
Dar-es-Salaam
T anzania

Tel: +255 222 773006, 2774420
Fax: +255 222 774420
E-mail: director.tie@tie.go.tz
Website: www.tie.go.tz

## IDHINI

Mafunzo ya Ualimu wa Elimu ya Msingi Ngazi ya Cheti ni ya miaka miwili na yamekusudiwa kuandaa walimu mahiri wenye uwezo wa kufanya kazi kwa dhati. Walimu hao watafundisha katika shule za msingi. Mwalimu mwanafunzi atatambuliwa kuwa ni mwalimu baada ya kuhudhuria na kufaulu mafunzo ya cheti ya miaka miwili ambamo pia atafanya na kufaulu mazoezi ya kufundisha.

Andiko hili linaidhinishwa kuwa ni **Muhtasari wa Ualimu Elimu kwa Michezo Mafunzo ya Ualimu wa Elimu ya Msingi Ngazi ya Cheti** wa mwaka 2009.

Umeidhinishwa na ......................................................

Saini...............................................................................

Tarehe...................................................................2009

**Kamishna wa Elimu**
Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi
S.L.P. 9121
**Dar-es-Salaam**

**Simu: +255 222 110150,110179, 110146**
**Nukushi: +255 222 113271**
**Tovuti: www.moe.go.tz**

## YALIYOMO


| | | Ukurasa |
|---|---|---|
| Utangulizi………………………………………………………………………. | | iv |
| Maelezo kuhusu muhtasari wa somo la Ualimu………………………….. | | iv |
| Sababu za kuwa na muhtasari huu……………………………………….. | | iv |
| Madhumuni ya Kufundisha Somo ............................................................ | | iv |
| Ujuzi wa Somo la Ualimu wa Elimu kwa Michezo……………………… | | v |
| Malengo ya Somo la Ualimu wa Elimu kwa Michezo Ngazi ya Cheti | | vi |
| Muundo wa Muhtasari wa Somo la Ualimu wa Elimu kwa Michezo…… | | vi |
| Upimaji na Tathmini ..................................................................................... | | vii |
| Muda wa Mafunzo......................................................................................... | | viii |
| **1.0** | **MISINGI YA ELIMU……………………………………………** | 1 |
| | 1.1 Dhana ya Elimu na Elimu kwa Michezo ……………………... | 1 |
| | 1.2 Falsafa ya Elimu Kwa Michezo……………………………….. | 2 |
| | 1.3 Sosholojia ya Elimu Kwa Michezo……………………………. | 3 |
| | 1.4 Uongozi na Utawala wa Elimu Tanzania……………….......... | 3 |
| | 1.5 Maadili ya Ualimu…………………………………………….. | 4 |
| **2.0** | **SAIKOLOJIA .......................................................................** | **5** |
| | 2.1 Dhana ya Saikolojia ya Elimu kwa MIchezo ............................. | 5 |
| | 2.2 Makuzi na Ukuaji wa Mtoto...................................................... | 6 |
| | 2.3 Nadharia ya Kujifunza ..............................................................  | 7 |
| | 2.4 Motisho katika Ujifunzaj............................................................ | 8 |
| **3.0** | **USHAURI NA UNASIHI...............................................................** | **8** |
| | 3.1 Dhana ya ushauri na Unasihi...................................................... | 8 |
| | 3.2 Kanuni za Unasihi........................................................................ | 9 |
| **4.0** | **MITAALA………………………………………………………….** | **10** |
| | 4.1 Dhana ya Mtaala………………………………………………… | 10 |
| | 4.2 Uandaaji wa Mtaala……………………………………………… | 11 |
| **5.0** | **UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI………………………………** | **11** |
| | 5.1 Dhana ya Ufundishaji na Ujifunzaji…………………………… | 11 |

5.2 Misingi Fanisi ya Ufundishaji na ujifunzaji Elimu ya Michezo 12
5.3 Matayarisho ya Ufundishaji………………………………………. 13
5.4 Mazoezi ya ufundishaji………………………………………… 14

**6.0 UTAFITI........................................................................................ 15**
6.1 Dhana ya utafiti.............................................................................. 15
6.2 Hatua za Utafiti.............................................................................. 16

**7.0 UPIMAJI ........................................................................................ 16**
7.1 Dhana ya Upimaji............................................................................ 16
7.2 Nyanja za Upimaji............................................................................ 17
7.3 Zana za Upimaji................................................................................ 18
7.4 Utungaji wa Maswali......................................................................... 19

**8.0 TATHMINI.......................................................................................... 20**
8.1 Dhana ya Tathimini........................................................................ 20
8.2 Ufasiri wa Matokeo ya Mitihani..................................................... 21
8.3 Uchambuzi wa Matokeo ya Mitihani............................................. 22
8.4 tathimini ya Mtaala......................................................................... 23

Rejea .......................................................................................................... 24

## UTANGULIZI

Muhtasari wa Somo la Ualimu Ngazi ya Cheti Elimu kwa Michezo umeandaliwa kwa ajili ya mwanachuo wa Ualimu anayejiandaa kufundisha Elimu kwa Michezo katika Shule za Msingi.

**Maelezo kuhusu muhtasari**

Muhtasari huu umeunganisha maudhui muhimu kutoka katika masomo ya ualimu, yaani, Misingi ya Ualimu, Saikolojia ya Elimu, Mitaala, Ufundishaji, Utafiti, Upimaji na Tathmini. Muunganisho huu unalenga kupunguza idadi ya masomo yatakayosomwa katika kozi ya Ualimu wa Elimu kwa Michezo.

**Sababu za kuwa na Muhtasari huu**

Muhtasari huu umeandaliwa kumwezesha kila mwanachuo wa ualimu ngazi ya cheti Elimu kwa Michezo kuielewa kazi yake kinadharia na kivitendo. Muhtasari huu umeandaliwa kwa mara ya kwanza. Kuanzishwa kwa muhtasari huu unatokana na uamuzi wa Serikali wa mwaka 2007 kuimarisha mafunzo ya ualimu katika nyanja ya Elimu kwa Michezo pamoja na ule uamuzi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi 2008 wa kuimarisha mafunzo ya ualimu na kutatua tatizo la upungufu wa walimu ngazi ya cheti linalokabili nchi kwa ujumla. Hii ni pamoja na kukidhi mahitaji na idadi ya walimu kutokana na kupanuka kwa sekta ya elimu ya msingi kufuatia kutekelezwa kwa mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM), kuongezeka kwa mahitaji ya walimu wenye kiwango cha juu cha taaluma na utaalam na kushughulikia masuala mtambuko.

**Madhumuni ya Mafunzo ya Ualimu wa Elimu kwa Michezo Ngazi ya Cheti**

Mafunzo ya ualimu hapa nchini yana madhumuni yafuatayo:

a) Kuwezesha wanachuo kupata nadharia ya saikolojia ya elimu na kunasihi.
b) Kuwawezesha wanachuo kupata stadi mbalimbali za kufundishia na kujifunzia.
c) Kukuza uelewa na uchambuzi wa mitaala itumikayo katika shule za msingi.
d) Kukuza na kuendeleza utaalam wa kufundisha masomo ambayo wanachuo watatakiwa kuyafundisha.

e) Kuwajengea wanachuo stadi na ujuzi wa kufanya utafiti wa kielimu, upimaji na tathmini.
f) Kukuza uwezo wa wanachuo katika uongozi na utawala wa kielimu.
g) Kukuza uwezo wa wanachuo juu ya kushughulikia masuala mtambuko.
h) Kuwajengea wanachuo uwezo wa kutumia teknolojia iliyopo katika mchakato wa kufundisha na kujifunza

**Ujuzi wa somo la Ualimu wa Elimu kwa Michezo Ngazi ya Cheti**

Baada ya miaka miwili ya mafunzo ya ualimu ngazi ya cheti, mwanchuo aweze kuonesha kanuni za msingi, stadi na mwelekeo katika:

a) Kupanga na kuendesha mchakato wa ufundishaji wa Elimu kwa Michezo.
b) Kupima na kutathmini maendeleo ya ufundishaji wa Elimu kwa Michezo.
c) Kupanga na kusimamia darasa la Elimu kwa Michezo
d) Kufanya tafiti mbalimbali kwa lengo la kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa Elimu kwa Michezo
e) Kushauri na kunasihi wanafunzi wenye mahitaji tofauti ya ujifunzaji katika Elimu kwa Michezo
f) Kubuni,kuunda na kutumia zana za kufundishia na kujifunzia katika somo la elimu kwa michezo

**Malengo ya Somo la Ualimu wa Elimu kwa Michezo Ngazi ya Cheti**

Baada ya mafunzo ya miaka miwili ya ualimu ngazi ya cheti ualimu wa Elimu kwa Michezo mwanachuo aweze:

a) Kupanga, kusimamia, na kuongoza, ufundishaji na ujifunzaji wa darasa la Elimu kwa Michezo.
b) Kutayarisha na kutumia vifaa vya mtaala wa Elimu kwa Michezo katika ufundishaji
c) Kutumia nadharia za Elimu kwa Michezo na kuzitafsiri katika mazingira halisi
d) Kuwa mbunifu katika kuumba, kufaragua, kutengeneza na kutumia vifaa vya kufundishia na kujifunzia Elimu kwa Michezo kwa kutumia rasilimali zilizopo kwenye mazingira yanayomzunguka.
e) Kupata maarifa na ujuzi wa kutumia vifaa/zana katika ufundishaji na ujifunzaji wa darasa jumuishi.

f) Kuwatambua watoto wenye mahitaji maalum na kubuni mbinu za kuwasaidia wajifunze vizuri.
g) Kupata maarifa na stadi ya uongozi na utawala wa Elimu kwa Michezo
h) Kutumia kanuni za msingi za falsafa na sosholojia katika Elimu kwa Michezo
i) Kutumia kanuni za ushauri na unasihi katika Elimu kwa Michezo
j) Kutumia mbinu za kitafiti katika Elimu kwa Michezo kwa lengo la kuboresha ufundishaji na ujifunzaji
k) Kufanya upimaji na tathmini kuhusu Elimu kwa Michezo

**Muundo wa Muhtasari wa Somo la Ualimu Elimu kwa Michezo Ngazi ya Cheti**

Muhtasari huu umepangiliwa kutokana na mkusanyiko wa mada kutoka katika masomo ya utaalamu yaani; Misingi ya Elimu, Saikologia ya Ualimu, Mitaala na Ufundishaji pamoja na Elimu ya Utafiti, Upimaji na Tathimini. Mada kuu zote zinatokana na masomo hayo. Mada ndogo ni mtiririko wa vipengele vya masomo hayo na katika kila mada kuu kuna mada ndogo zaidi ya moja. Kila mada ndogo ina malengo mahususi yanayoonesha matarajio yaliyokusudiwa kuwafikia walengwa. Na kwa kila mada ndogo kumependekezwa mbinu mbalimbali za kufundishia na kujifunzia, zana za/vifaa vya kujifunzia na kujifunzia na taratibu za upimaji. Mwisho muhtasari huu umeorodhesha rejea mbalimbali zilizotumika katika kuandaa muhtasari.

**Upimaji na Tathmini ya Maendeleo ya Mwanachuo**

Wanachuo watapimwa mara kwa mara kwa kutumia mbinu anuwai za upimaji ili kufahamu maendeleo ya ujifunzaji wao. Upimaji huu utakuwa katika makundi makuu mawili – Upimaji Endelezi ambao utakuwa na jumla ya alama **50%** na Upimaji tamati utakaohusisha mitihani ya mwisho inayotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA) nao utakuwa na jumla ya alama **50%.** Mazoezi ya kufundisha (BTP) yatapimwa kwa kuzingatia taratibu za Baraza la Mitihani la Taifa.

**Jedwali la Upimaji Endelezi**

| **Na** | **Mbinu za Upimaji** | **Mrundiano** | **Alama** |
|---|---|---|---|
| 1 | Uwasilishaji darasani | 4 | 10% |
| 2 | Kazi mradi/projekti | 1 | 10% |
| 3 | Majaribio | 4 | 10% |
| 4 | Mkoba wa Kazi | 4 | 5% |
| 5 | Mitihani ya Muhula | 3 | 15% |
| | **Jumla** | | **50%** |

**Muda wa Mafunzo**

Muda wa mafunzo ya Ualimu Ngazi ya Cheti ni miaka miwili (2), ambapo mwanachuo atapata mafunzo hayo akiwa chuoni. Somo hili limepangiwa muda wa saa mbili (2) tu kwa wiki

Mazoezi ya ufundishaji (BTP) yatafanyika katika muhula wa pili mwaka wa kwanza kwa muda wa wiki nne (4) na muhula wa pili mwaka wa pili kwa muda wa wiki nne(4). Katika kipindi chote cha mafunzo chuoni, mkufunzi anatakiwa azingatie umuhimu wa muda uliopangwa ili kufikia malengo tarajiwa.

## 1.0 MISINGI YA ELIMU KWA MICHEZO

### 1.1 Dhana ya Elimu na Elimu kwa Michezo

**Muda:** Saa 5

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada hii ndogo, mwanachuo aweze:-

a) Kufafanua dhana ya elimu na elimu kwa michezo.
b) Kueleza umuhimu wa elimu na elimu kwa michezo
c) Kutofautisha aina kuu za elimu
d) Kuchambua misingi ya elimu kwa michezo,
e) Kulinganisha historia na ukuaji wa elimu kwa michezo

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Bungua bongo
b) Majadiliano ya vikundi.
c) Maswali na majibu.
d) Fikiri jozisha shirikisha
e) Maswali na majibu.
f) Igizo dhima kuaridhia Elimu kwa Michezo katika kuimarisha mshikamano, upendo, amani na ushirikiano.

**Zana za/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

Vitabu na machapisho mbalimbali ya elimu**,** Vipeperushi , Chati mbalimbali za Elimu, Mtandao wa kompyuta, Kanda za video, DVD

**Upimaji**

a) Jaribio
b) Zoezi.
c) Kazi mradi.

### 1.2 Falsafa ya Elimu kwa Michezo

**Muda:** Saa 7

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada hii ndogo, mwanachuo aweze:-

a) Kufafanua dhana ya falsafa ya elimu kwa michezo,
b) Kuaridhia umuhimu wa falsafa ya elimu kwa michezo.
c) Kuchambua michango mbalimbali ya wanafalsafa katika elimu kwa michezo.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Bungua bongo.
b) Majadiliano katika vikundi.
c) Kazi za maktaba.

**Zana za/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Vitabu mbalimbali vya falsafa ya elimu kwa michezo.
b) Chati inayoelezea michango ya wanafalsafa
c) Video, DVD za kazi mbalimbali za wanafalsafa.

**Upimaji**

a) Zoezi.
b) Jaribio.

### 1.3 Sosholojia ya Elimu Kwa Michezo

**Muda:** Saa 4

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada hii ndogo, mwanachuo aweze:-

a) Kutoa fasili ya dhana ya sosholojia ya elimu kwa michezo
b) Kuelezea umuhimu wa sosholojia ya elimu kwa michezo.
c) Kubaini uhusiano wa elimu kwa michezo na siasa, elimu, afya, uchumi na masuala mtambuko.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Bungua bongo.
b) Majadiliano ya vikundi.
c) Mhadhara shirikishi na kazi za maktaba.

d) Mkoba wa kazi katika kuelezea uhusiano uliopo kati ya Elimu kwa Michezo na Siasa, Elimu, Afya, Uchumi na Jamii.

**Zana za/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

Vitabu na machapisho mbalimbali ya elimu**,** Vipeperushi , Kanda za video, DVD**,** Machapisho ya Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Michezo na elimu kwa michezo kwa maendeleo na tovuti mbalimbali za kitaaluma.

**Upimaji**

a) Kazi binafsi, zoezi, fomu ya uchunguzi, fomu ya ulinganifu wa viwango.
b) Mkoba wa kazi katika kuelezea uhusiano uliopo kati ya Elimu kwa Michezo na Siasa, Elimu, Afya, Uchumi na Jamii

## 1.4 Uongozi na Utawala wa Elimu Tanzania

**Muda:** Saa 3

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada hii ndogo, mwanachuo aweze:-

a) Kuelezea dhana ya uongozi na utawala wa elimu Tanzania.
b) Kuainisha aina za uongozi.
c) Kuchambua misingi uongozi,
d) Kuelezea muundo wa uongozi wa elimu Tanzania

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Fikiri jozisha shirikisha dhana, aina ya uongozi na utawala.
b) Majadiliano ya vikundi kueleza misingi ya uongozi
c) Kazi mradi kuhusu muundo wa uongozi wa elimu kwa ngazi ya shule, kata, wilaya, mkoa hadi taifa.

**Zana za/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

Kanda za video, DVD, CD kuhusu uongozi wa Elimu ,Vitabu mbalimbali vya uongozi na utawala na Chati za muundo wa Elimu Tanzania.

**Upimaji**

a) Majaribio
b) Mazoezi, insha na fomu ya ulinganifu wa viwango.
c) Orodha hakiki.

## 1.5 Maadili ya Ualimu

**Muda:** Saa 4

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada hii ndogo, mwanachuo aweze:-

a) Kuelezea dhana ya maadili ya ualimu.
b) Kufafanua umuhimu wa maadili ya ualimu.
c) Kuaridhia uhusiano wa ualimu na maisha ya kila siku katika jamii

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Bungua bongo.
b) Majadiliano ya vikundi.
c) Mhadhara shirikishi.
d) Kumwalika mgeni kuelezea maadili ya ualimu na umuhimu wake katika kazi na jamii.

**Zana za/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

Vitabu mbalimbali vya maadili ya Utumishi.

**Upimaji**

Mazoezi, insha, fomu ya uchunguzi na orodha hakiki.

## 2.0 SAIKOLOJIA YA ELIMU KWA MICHEZO

### 2.1 Dhana ya Saikolojia ya Elimu kwa Michezo

**Muda:** Saa 3

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada hii ndogo, mwanachuo aweze:-

a) Kulezea dhana ya Saikolojia na Saikolojia ya Michezo.
b) Kubainisha umuhimu wa Saikolojia katika Michezo
c) Kuchambua nadharia mbalimbali za kupata maarifa ya Saikolojia ya Elimu kwa Michezo.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Fikiri jozisha shirikisha.
b) Majadiliano katika vikundi.
c) Kazi za maktaba.

**Zana za/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

Vitabu vya saikolojia, Vitabu vya saikolojia ya michezo, Majarida ya michezo

**Upimaji**

a) Mazoezi
b) Kazi binafsi
c) Mkoba wa kazi .

### 2.2 Makuzi na Ukuaji wa Mtoto

**Muda:** Saa 6

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada hii ndogo, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza dhana ya makuzi na ukuaji wa mtoto.
b) Kuainisha aina za makuzi na ukuaji wa mtoto.
c) Kufafanua mambo yanayoathiri ukuaji na makuzi ya mtoto.
d) Kubainisha watoto wenye mahitaji maalumu.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Bungua bongo.
b) Majadiliabo katika vikundi
c) Fikiri jozisha shirikisha.
d) Kutumia kadi za NDIYO na HAPANA kueleza dhana ya watoto wenye mahitaji maalum.
e) Maswali na majibu.

**Zana za/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

Mabango juu ya ukuaji wa mtoto, Vitabu/majarida yanayohusu ukuaji na makuzi ya mtoto, Chati za hatua za ukuaji wa mtoto, Picha za watoto wenye mahitaji maalum, Maazimio mbalimbali ya kimataifa kuhusu watoto wenye mahitaji maalum.

**Upimaji**

a) Mazoezi
b) Zoezi.
c) Mkoba wa kazi.

**2.3 Nadharia ya Kujifunza**

**Muda:** Saa 8

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada hii ndogo, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza dhana ya Kujifunza katika Elimu kwa Michezo.
b) Kuanisha nyanja na kanuni za kujifunza.
c) Kupambanua nadharia za kujifinza
d) Kufafanua dhana ya kukumbuka na kusahau

**Mbinu za kufundisha/kujifunzia**

a) Bungua bongo.
b) Kazi za maktaba.
c) Maswali na majibu
d) Mjadala juu ya mbinu za kujenga kumbukumbu

**Zana za/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

Vitabu/majarida yanayohusu kujifunza, projekta.

**Upimaji**

a) Maswali ya mdomo juu ya insha.
b) Zoezi.
c) Kazi binafsi.

## 2.4 Motisho katika ujifunzaji

**Muda:-** Saa 5

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada hii ndogo, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza maana ya Motisha na Vichocheo.
b) Kubainisha aina za Motisha na Vichocheo.
c) Kutathmini matumizi ya Motisha na Vichocheo katika Michezo
d) Kufafanua umuhimu wa uhawilishaji wa maarifa katika kujifunza michezo

**Mbinu za kufundishi/kujifunzia**

a) Fikiri jozisha shirikisha.
b) Mjadala juu ya aina na matumizi ya motisho na vichocheo katika michezo.
c) Maswali na majibu.

**Zana za/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

Vitabu vya saikolojia na Vitabu/majarida yanayohusu motisho na motisho katika michezo

**Upimaji**

a) Maswali mafupi
b) Kazi binafsi.

## 3.0 USHAURI NA UNASIHI

**Muda:** Saa 4

### 3.1 Dhana ya Ushauri na Unasihi

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada hii ndogo, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza dhana ya ushauri na unasihi.
b) Kuaridhia umuhimu wa ushauri na unasihi.
c) Kuchanganua aina na hatua za unasihi.
d) Kubainisha changamoto wakati wa ushauri na unasihi.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Fikiri, jozisha shirikisha.
b) Maswali na majibu.
c) Majadiliano katika vikundi.
d) Kazi za maktaba.
e) Igizo dhima.

**Zana za/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

Vitabu vya ushauri na unasihi, Kanda za video zinazoonesha tendo la kushauri na kunasihi, kanda za redio zinazohusu unasihi na ushauri, chati ya mbinu za ushauri na unasihi na kanda za video zioneshazo unasihi na ushauri michezoni.

**Upimaji**

a) Maswali mafupi
b) Mkoba wa kazi na fomu ya ulinganifu wa viwango.

### 3.2 Kanuni za Unasihi

**Muda: 6**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada hii ndogo, mwanachuo aweze:-

a) Kuchambua sifa za mnasihi
b) Kubainisha mazingira/nyakati yanayohitaji unasihi katika Michezo.

c) Kuonesha Ujuzi wa kunasihi
d) Kutumia mbinu za kunasihi

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Maswali na majibu
b) Fikiri, jozisha shirikisha.
c) Onesho mbinu katika kutumia ujuzi na mbinu mbalimbali za kunasihi michezoni.

**Zana za/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

Vitabu vya ushauri na unasihi, Kanda za video zinazoonesha tendo la kushauri na kunasihi, Kanda za redio zinazohusu unasihi na ushauri., Chati ya mbinu za ushauri na unasihi na Kanda za video zioneshazo unasihi na ushauri michezoni.

**Upimaji**

a) Maswali mafupi.
b) Mkoba wa kazi.

## 4.0 MITAALA

### 4.1 Dhana ya Mtaala

**Muda:** Saa 3

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada hii ndogo, mwanachuo aweze:-

a) Kuelezea dhana ya mitaala ya elimu.
b) Kubaini umuhimu wa mitaala katika elimu
c) Kufafanua aina za mitaala

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Majadiliano katika vikundi.
b) Maswali na majibu.
c) Fikiri jozisha shirikisha.

**Zana za/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

Mihtasari mbalimbali, Vitabu vinavyoelezea mitaala na makala/matini zinazohusu mtaala kutoka katika mtandao.

**Upimaji**

a) Maswali ya mdomo, insha.
b) Kazi binafsi
c) Zoezi.

### 4.2 Uundaji wa mtaala

**Muda: 7**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada hii ndogo, mwanachuo aweze:-

a) Kubainisha modeli mbalimbali katika uundaji wa mtaala.
b) Kuelezea dhana ya shabaha, madhumuni na malengo katika mtaala.
c) Kuchanganua vifaa vya mtaala.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Majadiliano katika vikundi.
b) Maswali na majibu.
c) Kazi ya maktaba.

**Zana za/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

Mihtasari mbalimbali**,** chati inayoonesha vipengele vya mitaala, vitabu**,** makala kutoka katika mtandao wa kompyuta**,** machapisho mbalimbali yanayozungumzia vipengele vya mtaala.

**Upimaji**

a) Maswali mafupi.
b) Zoezi.

## 5.0 UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI

### 5.1 Dhana ya ufundishaji na ujifunzaji

**Muda:** Saa 4

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada hii ndogo, mwanachuo aweze:-

a) Kuelezea dhana ya ufundishaji na ujifunzaji.
b) Kuchanganua njia/mbinu za ufundishaji na ujifunzaji,
c) Kuchambua nadharia ya kujifunza

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Maswali na majibu.
b) Majadiliano na kuwasilisha.
c) Kazi ya maktaba.

**Zana /vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

Vitabu mbalimbali vinavyozungumzia ufundishaji. Majarida na machapisho, chati inayoonesha mbinu na njia za kufundishia., Kanda za video zinazoonesha ufundishaji.

**Upimaji**

a) Maswali ya mdomo, insha.
b) Zoezi.
c) Kazi

### 5.2 Misingi fanisi ya ufundishaji na ujifunzaji elimu kwa michezo

**Muda: 5**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada hii ndogo, mwanachuo aweze:-

a) Kuelezea dhana ya misingi fanisi ya ufundishaji na ujifunzaji
b) Kufafanua misingi ya ufundishaji na ujifunzaji kama ilivyoainishwa na Farrant (1992)
c) Kuelezea usimamizi na utawala wa darasa la elimu kwa michezo
d) Kutumia ufundishaji na ujifunzaji akisi

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia.**

a) Bungua bongo, maswali na majibu.
b) Kazi ya maktaba/ tovuti.
c) Maswali na majibu.
d) Fikiri jozisha shirikisha.

**Zana za/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

Vitabu, majarida na machapisho, chati inayoonesha mbinu na njia za kufundishia, kanda za video zinazoonesha ufundishaji

**Upimaji**

a) Maswali mafupi
b) Kazi binafsi, insha.
c) Fomu ya uchunguzi, orodha hakiki.
d) Zoezi

**5.3 Matayarisho ya Ufundishaji**

**Muda:** Saa 5

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada hii ndogo, mwanachuo aweze:-

a) Kuelezea dhana ya Azimio la kazi, Andalio la somo, Nukuu za somo na shajara
b) Kubaini vipengele vya Azimio la kazi, Andamio la somo, Nukuu za somo na shajara
c) Kuandaa Azimio la somo, Andalio la somo na shajara
d) Kuandaa zana/vifaa vya kufundishia na kujifunzia

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Bungua bongo.
b) Fikiri jozisha shirikisha.
c) Majadiliano kwa vikundi.
d) Andalio la somo, Nukuu za somo na Shajara.
e) Kazi za maktaba kuainisha vipengele vya Andalio la Somo.

f) Majadiliano katika vikundi na kuandaa Andalio la Somo.
g) Bungua bongo na maswali na majibu kuelezea faida za andalio la somo.
h) Majadiliano katika vikundi, kuandaa zana/vifaa vya kufundishia.
i) Majadiliano katika vikundi kuelezea umuhimu wa vifaa na zana za kufundishia.

**Zana /vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

Mihtasari mbalimbali, Azimio la kazi, Andalio la somo, Zana mbalimbali (mipira, filimbi), Nukuu za somo, Shajara

**Upimaji**

a) Jaribio.
b) Majibu ya mdomo.
c) Zoezi
d) Mkoba wa kazi

### 5.4 Mazoezi ya Kufundisha

**Muda : Saa 5**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada hii ndogo, mwanachuo aweze:-

a) Kuelezea Dhana ya Mazoezi ya Kufundisha
b) Kuchanganua aina za mazoezi ya kufundisha (ufundishaji rika, ufundishaji kiduchu, ufundihsaji wa muda mfupi, na ufundishaji wa muda mrefu)
c) Kubaini umuhimu wa mazoezi ya kufundisha
d) Kuandaa mazoezi ya kufundisha.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Bungua bongo, maswali na majibu.
b) Mhadhara shirikishi.
c) Majadiliano katika vikundi.
d) Kazi binafisi kuandaa mazoezi ya kufundisha.

**Zana za/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

Mihtasari mbalimbali ya masomo, Azimio la kazi, Andalio la somo, Zana mbalimbali (mipira, filimbi), Nukuu za somo na Shajara

**Upimaji**

a) Mazoezi, insha.
b) Kazi mradi kuandaa azimio na andalio la somo
c) Mkoba wa kazi, orodha hakiki.

## 6.0 UTAFITI

### 6.1 Dhana ya Utafiti

**Muda: 4**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada hii ndogo, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza maana ya Utafiti wa Elimu
b) Kuainisha aina za utafiti wa kielimu.
c) Kuaridhia umuhimu wa utafiti katika Elimu ya Michezo

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Bungua bongo.
b) Majadiliano katika vikundi.
c) Kazi za maktaba.

**Zana /vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

Vitabu vya utafiti, ripoti za tafiti mbalimbali.

**Upimaji**

a) Mazoezi, insha
b) Jaribio

### 6.2 Hatua za Kufanya Utafiti

**Muda : 6**

**Malengo Mahsusi**

**Baada ya kukamilisha mada hii ndogo, mwanachuo aweze:-**

a) Kufafanua hatua za kufanya utafiti.
b) Kubaini zana za utafiti.
c) Kuandaa zana za utafiti.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Maswali na majibu.
b) Majadiliano ya vikundi.
c) Kazi mradi kuandaa zana za utafiti.

**Zana /vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

Sampuli za miongozo ya usaili, maswali ya dodoso, maswali ya orodha hakiki na ripoti za utafiti

**Upimaji**

a) Jaribio.
b) Mazoezi.
c) Mkoba wa kazi

## 7.0 UPIMAJI

### 7.1 Dhana ya Upimaji

**Muda:** Saa 3

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada hii ndogo, mwanachuo aweze:-

a) Kuelezea maana ya Upimaji.
b) Kuainisha aina za upimaji.
c) Kubainisha umuhimu wa upimaji katika elimu kwa michezo.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Bungua bongo.
b) Mhadhara shirikishi.
c) Maswali na majibu kuainisha aina za upimaji
d) Majadiliano ya vikundi.

**Zana za/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

Vitabu vya upimaji katika elimu, ripoti za mitihani, ripoti za wakaguzi wa shule, fomu za maendeleo ya kila siku, chati za jedwali la kutahini

Sampuli za maswali ya jaribio/mitihani mbalimbali, sampuli za muundo wa mitihani, mwongozo wa baraza la mitihani kuhusu utungaji wa mitihani

**Upimaji**

a) Maswali mafupi
b) Zoezi
c) Fomu ya ulinganifu wa viwango.

## 7.2 Nyanja za Upimaji

**Muda:** Saa 5

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada hii ndogo, mwanachuo aweze:-

a) Kuelezea nyanja za upimaji.
b) Kuainisha ngazi za nyanja za upimaji.
c) Kubainisha vitenzi vinavyotumika katika ngazi za upimaji.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Maswali na majibu.
b) Majadiliano katika vikundi kazi za maktaba.
c) Maswali na majibu kubainisha vitenzi vinavyotumika katika ngazi za upimaji.

**Zana za/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

Vitabu vya upimaji katika elimu, chati za jedwali la kutahini, sampuli za maswali ya jaribio/mitihani mbalimbali na sampuli za muundo wa mitihani

**Upimaji**

a) Maswali mafupi
b) Zoezi.
c) Mkoba wa kazi

## 7.3 Zana za Upimaji

**Muda 3**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada hii ndogo, mwanachuo aweze:-

a) Kuelezea maana ya zana za upimaji.
b) Kubainisha aina na umuhimu wa zana za upimaji katika michezo.
c) Kufafanua matumizi ya zana za upimaji.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Bungua bongo.
b) Kazi za maktaba.
c) Mjadala shirikishi.
d) Fikiri jozisha shirikisha.

**Zana za/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

Vitabu, Sampuli za maswali ya jaribio/mitihani mbalimbali.
Sampuli za muundo wa mitihani.

**Upimaji**

a) Maswali ya mdomo
b) Zoezi
c) Kazi binafsi, mkoba wa kazi.

## 7.4 Utungaji wa Maswali

**Muda:** Saa 5

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada hii ndogo, mwanachuo aweze:-.

a) Kupambanua aina za maswali
b) Kuchambua sifa za maswali bora.
c) Kuelezea hatua za kufuata katika kutunga maswali bora.
d) Kuandaa jedwali la utahini.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Majadiliano katika vikundi.
b) Maswali na majibu.
c) Kazi za maktaba.
d) Fikiri jozisha shirikisha.

**Zana za/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

Vitabu vya upimaji katika elimu, ripoti za mitihani, ripoti za wakaguzi wa shule, mwongozo wa baraza la mitihani kwa watahiniwa, fomu za maendeleo ya kila siku, chati za jedwali la kutahini, sampuli za maswali ya jaribio/mitihani mbalimbali, Sampuli za muundo wa mitihani na mwongozo wa baraza la mitihani kuhusu utungaji wa mitihani

**Upimaji**

a) Mazoezi.
b) Majaribio.
c) Zoezi.
d) Mkoba wa kazi

## 8.0 TATHMINI

### 8.1 Dhana ya Tathmini

**Muda:** Saa 3

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada hii ndogo, mwanachuo aweze:-

a) Kuelezea dhana ya Tathmini.
b) Kuaridhia umuhimu wa tathmini
c) Kuchambua aina ya tathimini
d) Kubaini umuhimu wa tathimini ya elimu kwa michezo.
e) Kutofautisha kati ya upimaji na tathmini.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Fikiri jozisha shirikisha.
b) Majadiliano katika vikundi, kazi za maktaba.

**Zana za/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

Majarida ya tathmini, majarida ya upimaji katika elimu na Elimu kwa Michezo, ripoti za maendeleo ya wanafunzi na Elimu kwa Michezo, ripoti za tathmini zilizoandikwa na wanachuo na ripoti za tathmini katika elimu.

**Upimaji**

Maswali mafupi, zoezi, kazi binafsi na mkoba wa kazi

### 8.2 Ufasiri wa matokeo ya mitihani

**Muda:** Saa 5

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada hii ndogo, mwanachuo aweze:-

a) Kubaini aina za ufasiri wa matokeo.
b) Kuelezea aina za ufasiri wa matokeo.
c) Kutofautisha kanuni za ufasiri wa matokeo.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Bungua bongo
b) Majadiliano katika vikundi.
c) Onyesho mbinu kutofautisha kanuni za ufasiri wa matokeo.

**Zana za/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

Vitabu vya upimaji katika elimu, ripoti za mitihani, ripoti za wakaguzi wa shule, mwongozo wa baraza la mitihani kwa watahiniwa, fomu za maendeleo ya kila siku, chati za jedwali la kutahini, sampuli za maswali ya jaribio/mitihani mbalimbali, sampuli za muundo wa mitihani na mwongozo wa baraza la mitihani kuhusu utungaji wa mitihani

**Upimaji**

a) Zoezi, insha, mkoba wa kazi.
b) Majaribio.

## 8.3 Uchambuzi wa matokeo ya mtihani

**Muda:** Saa 6

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada hii ndogo, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza maana ya uchambuzi wa matokeo.
b) Kuaridhia umuhimu wa uchambuzi matokeo.
c) Kuainisha data, na vyanzo vya kukusanya data.
d) Kuchanganua njia na mbinu za kukusanya data.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Fikiri jozisha shirikisha.
b) Majadiliano katika vikundi
c) Kazi za maktaba.

**Zana za/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

Majarida ya tathmini, majarida ya upimaji katika elimu na Elimu kwa Michezo, ripoti za maendeleo ya wanafunzi na Elimu kwa Michezo, ripoti za tathmini zilizoandikwa na wanachuo na Ripoti za tathmini katika elimu.

**Upimaji**

Maswali mafupi, insha

Kazi mradi na fomu ya ulinganifu wa viwango.

**8.4. Tathmini ya Mtaala**

**Muda:** Saa 4

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada hii ndogo, mwanachuo aweze:-

a) Kuchambua hatua za kuzingatia wakati wa kufanya tathmini ya mtaala.
b) Kubainisha vipengele vya tathmini ya mtaala.
c) Kutathmini vifaa vya mtaala

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

Fikiri jozisha shirikisha.

Majadiliano katika vikundi.

Kazi za maktaba

**Zana za/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

Mihutasri mbali mbali ya masomo, Rejea mbalimbali, Shajara, Mwongozo wa elimu, Sera ya Elimu

**Upimaji**

a) Maswali mafupi.
b) Kazi binafsi/nyumbani
c) Kazi mradi kuchambua na kutathimi vifaa vya mtaala.

**Rejea Zilizotumika**

Biswalo, P.M. (1996), Introduction to Guidance and Counselling in Diverse African Settings, Dar es Salaam: DUP.

Butcher, W. (1999) Foundations of Physical Education and Sport (13rd edn.), Boston: Mc Graw Hill

Dorothy, B.Z. *et a*l (1994). Quality Lesson Plans for Secondary Physical Education, Kinetics Champain Il.

Farrants, S. (1964), Principle and Practice of Foundation, London: Longman.

German College of Physical Culture Lerpsin 1985), Text book Selected Problems of Sports Psychology DHFK.

Gronlund, N.E. and Linn, R.L. (1990). Measurement and Evaluation in Teaching, New York: MacMillan Publishing Company.

MANTEP, (1995), Educational Management Handbook for Primary School Headteachers, Bagamoyo, MANTEP.

Nkongo J. and Nkongo, T. (1981), Misingi ya Elimu kwa Michezo, Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Potgreter, J.R. (1997), Sport Psychology: Theory and Practice, Stltenbosch: Institute for Sport and Movement Studies.

Smith, W. (1961), Sports for School; London: Thomas and Sons Ltd.

Snyder, E.E. and Spreitzer, E. (1978), Social Aspects of Sports, Englewood Cliffs, N.J.

Straub, W. F. (1978), Sports Pychology: An Athlete’s Behaviour – Movement Publication.

Taasisi ya Elimu Tanzania, (1994), Ukuzaji Mitaala na Kunasihi, Dar es Salaam, Taasisi ya Elimu Tanzania.

Taasisi ya Ukuzaji Mitaala (1992), Saikolojia ya Elimu, Dar es Salaam.

Thomas, R.I. *et al* ( 1988), Physical Education for Children, Illinois: Human Kinetics.

Taasisi ya Elimu Tanzania (2000), Upimaji na Utahini wa Maendeleo ya Mwanafunzi, Dar es Salaam, Macmillan Aidan.